TANGAZO LA SERIKALI Na. 719 la tarehe. 16/8/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16 (1))*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI YA MWAKA 2024

Jina

TS Na. 893 la 2023

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ya Mwaka 2024, na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ya Mwaka 2023 ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo Kuu".

Marekebisho ya aya ya 3

2. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika aya ya 3 kwa kuongeza tafsiri ya maneno kama ifuatavyo:

"mfanyabiashara" maana yake ni mtu, taasisi, kikundi cha watu, kampuni, kiwanda au shirika linalolima mazao kibiashara au linalonunua mazao kwa ajili ya biashara au matumizi mengine;

"bei ya kununua mazao moja kwa moja kutoka kwenye chanzo" au "at source at farm gate price" maana yake ni bei ya soko katika eneo ambalo mazao hupatikana;".

Dodoma,
5 Juni, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi -OR-Tamiseni*